

MBOLEA BORA KWA KILIMO ENDELEVU

Mbolea YETU



Tanzania

ISSN 2799-2039

Toleo Na. 06 - Julai - Desemba 2023



TFRA, Wadau waleta faraja kwa waathirika wa mafuriko Hanang

Namna matumizi ya mbolea yanavyostawisha vitunguu maji
– Uk.10



Wadau walioendeleza tasnia ya mbolea wajizolea tuzo
– Uk.17

UJUMBE WA MKURUGENZI MTENDAJI

Bila mbolea, usalama wa chakula uko hatarini

TUNAPOZUNGUMZIA umuhimu wa matumizi ya mbolea ili kuongeza tija katika kilimo chetu, tunazungumzia hatima ya taifa letu kwa miaka mingi ijayo, hasa kuhusu suala la usalama wa chakula na ustawi wa maisha ya Watanzania kuanzia ngazi ya familia hadi taifa.

Tukumbuke kwamba sisi wa kizazi cha leo wengi wetu hatutakuwepo miaka 50 ijayo kushuhudia yale yatakayotokea kwa wajukuu, vilembwe na vitukuu wetu. Kwa hakika, hiyo itakuwa dunia nyingine kwa uzao wetu. Kutakuwa na watu wengi katika eneo dogo la kilimo. Itakuwa ni changamoto kubwa kwa uzao wetu kuliko wakati mwingine katika historia ya mwanadamu!

Watanzania lazima tukubali ukweli kwamba dunia ijayo – kwa maana ya wingi wa watu – itakuwa dunia nyingine yenye mahitaji makubwa ya chakula.

Ndiyo maana sisi kama taasisi ya kilimo tunasitisiza umuhimu wa matumizi sahihi ya mbolea katika uzalishaji wa mazao mbalimbali kwa lengo la kurutubisha na kuboresha afya ya udongo ili kuzalisha mazao kwa wingi.

Katika dunia hii inayoshuhudia ongezeko kubwa la idadi ya watu, ambayo wataalam wanasema itakuwa na watu bilioni 9.7 ifikapo mwaka 2050, ni dhahiri kwamba ongezeko hili litasababisha mahitaji makubwa ya uzalishaji wa mazao mengi katika eneo dogo.

Kwa mfano, katika miaka ya 1960 ekari moja iliweza kuzalisha chakula cha kutosheleza watu wawili, lakini miaka miwili ijayo ekari hiyo moja itapaswa izalishe chakula cha kutosheleza watu watano. Hii maana yake ni kwamba tusipojiandaa vizuri kama taifa kuhusu suala la usalama wa chakula huenda watu wengi wakahangaika kwa tishio la janga la njaa.

Hali kadhalika, sababu nyingine muhimu ya kuweka mkazo kwenye matumizi ya mbolea inatokana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yanapunguza uhakika wa mavuno ya mazao mbalimbali ya chakula.

Pia ukuaji wa miji na miundombinu unachangia kupunguza eneo linalofaa kwa kilimo na hivyo eneo dogo linalobakia linatakiwa kutumika kwa ufanisi zaidi kwa matumizi sahihi ya mbolea.

Matumizi ya mbolea yanabeba umuhimu wa pekee linapokuja suala la uhifadhi wa mazingira ambapo kila mahali duniani kuna kelele nyingi za uharibifu unaotokana na shughuli za binadamu kama vile ukataji miti na uchomaji moto misitu.

Ni muhimu kwa wadau wa tasnia ya mbolea kuunga mkono juhudzi mahususi za serikali za kuwawezesha wakulima kutumia mbolea bora kwa gharama nafuu. Juhudi hizo zinalenga kuongeza tija ya uzalishaji, kuimarisha usalama wa chakula, upatikanaji wa malighafi za viwanda, ukuaji wa sekta ya kilimo na uchumi kwa ujumla wake.

Serikali imeelekeza nguvu katika kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vya kutengeneza mbolea ambapo kwa sasa kuna viwanda vya mbolea zo nchini vinavyoendelea na uzalishaji wa bidhaa hiyo. Kati ya viwanda hivyo, viwanda viwili ni vikubwa na viwanda 18 ni vya kati na vidogo.

Viwanda hivi vimeendelea kuchangia ongezeko la uzalishaji wa ndani kutoka tani 28,318 (2018/19) hadi kufikia tani 164,792 (2022/23), sawa na asilimia 25 ya mahitaji.

Ni imani ya TFRA kwamba wakulima wataitumia fursa ya serikali ya kutoa mbolea ya ruzuku kwa ajili ya kuimarisha shughuli zao za kilimo ili kiweze kuleta tija katika maisha yao na kwa uchumi wa taifa.



Joel Laurent
Mkurugenzi Mtendaji

BODI YA UHARIRI

JOEL LAURENT
- MWENYEKITI

MATILDA KASANGA
- KATIBU

DANIEL MAARIFA
- MJUMBE

RAYMOND KONGA
- MJUMBE

AZIZI MTAMBO
- MJUMBE

SALEHE KEJO
- MJUMBE

THERESIA SIRIWA
- MJUMBE

NURU MWASAMPETA
- MJUMBE

ALPHA NUHU
- MJUMBE

TAHARIRI

Mbolea imechochea ongezeko uzalishaji chakula

UKWELI kwamba matumizi sahihi ya mbolea yamechochea ongezeko la uzalishaji chakula sasa umeanza kudhihiri nchini. Hali hiyo ilijionyesha bayana wakati wa Maadhisho ya Siku ya Mbolea Duniani yaliyofanyika mjini Tabora Oktoba mwaka 2023.

Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk Batilda Burian, ni shuhuda ali-yethibitisha kwamba mkoa wake ni kipimo cha ongezeko la uzalishaji wa mazao ya chakula kutoka tani 973,106 mwaka 2021/2022 hadi tani 1,153,654 mwaka 2022/2023 kutokana na kichocheo cha matumizi ya mbolea.

Matumizi sahihi ya mbolea katika mkoa yanatajwa kuongeze-ka kutoka tani 41,995 mwaka 2021/2022 hadi tani 43,299 mwaka 2022/2023.

Kwa hakika, takwimu hizi, kwa mujibu wa Dk Burian, zinaakisi juhudzi zilizofanywa na zinazoendela kufanywa na serikali za kutoa ruzuku ya pembejeo na vitenda kazi kwa maafisa ugani.

Katika shamrashamra za Siku ya Mbolea Duniani Oktoba 13 zilizoambatana na maonesho ya wadau wa sekta ya mbolea, Dkt. Burian alieleza jinsi uzalishaji wa zao la biashara la Tumbaku amba-lo ni moja ya mazao ya kimkakati katika mkoa huo ulivyoongezeka kutoka kilo 29,815,082 mwaka 2021/2022 hadi kilo 62,964,460.83 mwaka 2022/2023 wakati bei ya wastani ikiongezeka kutoka dola za Marekani 1.81 kwa kilo hadi kufikia dola 2.3 katika kipindi hicho.

Kitakwimu ongezeko hilo ni sawa na asilimia 111 na asilimia 27 mtawalia. Mapato ya wakulima katika kipindi hicho pia yameongeze-ka kutoka dola za Marekani 54,017,356.88 hadi dola 144,732,352.99, sawa na ongezeko la asilimia 168.

Ongezeko la bei lilitokana na ujio wa kampuni mpya ya ununuzi wa Tumbaku ya Mkwawa Tobacco Leaf Limited mkoani humo ambayo kwa kiasi kikubwa imesaidia kuinua uchumi wa wakulima na mkoa kwa ujumla wake.

Baada ya kuonja matunda ya matumizi ya mbolea sasa mkoa wa Tabora umejipanga kuhakikisha kila wilaya inakuwa na vituo vya kutosha vya uuzaaji wa mbolea. Kwa sasa, mkoa huo una vituo 27 vya kuuzia mbolea ambayo ni idadi ndogo ikilinganishwa na matarajio ya kuwa na vituo 80.

Uwepo wa vituo vingi vya kuuzia mbolea utasaidia kuondoa changamoto ya wakulima kutembea umbali mrefu kutafuta pembejeo hiyo kama ilivyojitokeza katika misimu mingine mkoani humo.

Tumechukua mfano wa mkoa wa Tabora kuhusu matumizi ya mbolea ikiwa ni funzo maalum kwa wakulima nchi nzima: kwamba wakitumia pembejeo hiyo muhimu katika kilimo maisha yao kiuchumi yatabadilika haraka kwa kuondokana na umaskini uliokithiri.

Wakulima wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini – mikoa ya Iringa, Njombe, Ruvuma, Mbeya, Rukwa na Katavi --- wao ni mashuhuda kwamba matumizi ya mbolea yameufukuza umaskini uliokuwa uk-wakabili siku za nyuma.

Ni kutokana na ukweli huu ndiyo maana tunawahamasisha wakulima wote sasa waelekeze nguvu zao katika matumizi sahihi ya mbolea ili kujikwamua siyo tu na umaskini bali pia kujihakikisha usalama wa chakula katika taifa ambalo tangu uhuru limekuwa liki-shuhudia ongezeko kubwa la idadi ya watu.

ONGEZEKO UZALISHAJI CHAKULA



Rais Samia afurahishwa na ongezeko matumzi ya mbolea

Uk > 5



Wakaguzi wa Mbolea watakiwa kuwa waadilifu na weledi

Uk > 6



Serikali yataka wakulima kuhakiki taarifa kuhusu mbolea ya ruzuku maji

Uk > 7



Namna matumizi ya mbolea yanavyostawisha vitunguu maji

Uk > 10

Orodha ya Mbolea na Visaidizi vya Mbolea zilizosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Mbolea Na. 9 ya mwaka 2009

Uk > 18

TFRA, wadau waleta faraja kwa waathirika wa mafuriko Hanang

Na MWANDISHI WETU

KATIKA harakati za kuwasaidia wananchi wa wilaya ya Hanang mkoani Manyara ambao waliiathiri na mafuriko yaliyovuruga kwa kiasi kikubwa shughuli za kilimo, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) ikishiriki-

ana na wadau wa sekta hiyo ilikusanya tani 78.5 za mbolea zenyenye thamani ya 129,449,094/- na kuzikabidhi kwa viongozi wa Wilaya hiyo ili zigawie kama msaada kwa waathirika wa janga hilo la kitaifa.

Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Joel Laurent, alikabidhiwa tani 65 za mbolea za kupan-

dia na kukuzia mimea Desemba 7 mwaka jana (2023) ambazo zilitolewa na wazalishaji na wafanyabiasha wa mbolea nchini.

Tani 30 za mbolea zilitolewa na Kampuni ya Mbolea ya Taifa (TFC), tani 30 zilitoka Kampuni ya Uzalishaji wa Mbolea Itracom na 5 kutoka Kampuni ya Mbolea ya Minjingu.

Kwenye makabidhiano ya mbolea hizo, Laurent alieleza kwamba kampuni nyininge zilizotarajiwa kutoa msaada huo wa mbolea ni kampuni ya mbolea ya Staco -- tani 10, Yara -- tani 2.5 na kampuni ya Premium -- tani 1.

Aliwahamasisha wadau wengine wa mbolea kufikisha msaada yao kwa waathirika wakati huu wa msimu wa kilimo kwa sababu wakulima walikuwa wamenunua mbolea ambazo hazikuzaa matunda kutokana na janga la mafuriko.

Kwa mujibu wa Laurent, wakulima 8,449 waliosajiliwa Wilayani Hanang tayari walikuwa wameshanunua tani 1,131.2 za mbolea hadi wakati walipokumbwa na janga la mafuriko

TFRA yaweka mfumo thabiti mbolea za msaada kuwafikia walengwa

Laisema TFRA imeweka mfumo madhubuti kuhakikisha kwamba mbolea za msaada kwa waathirika wa mafuriko wilayani Hanang zinawafikia walengwa.

Alisema taarifa za wakulima waliojisajili katika eneo lilioathiriwa zipo na akatoa wito kwa wale ambao bado hawajajisajili kufanya hivyo ili kupata mbolea hizo.

Alieleza hayo Desemba 8 kwenye kituo cha kilimo alipokuwa akifanya makabidhiano maalum na Kamati ya Maafa kuititia Afisa Kilimo ya Wilaya ya Hanang, Liberatus Msasa.

Alisema ofisi ya Kilimo Wilayani Hanang itashirikiana na Ofisi ya TFRA Kanda ya Kaskazini kuhakikisha Afisa Kilimo anasajiliwa kama wakala na kuingiziwa mbolea hizo kwenye akaunti yake ili aweze kuzigawa kwa waathirika bure kwa utaratibu uliowekwa.

Mkurugenzi wa Uzalishaji wa Ndani na Ununuvi wa Mbolea kwa Pamoja wa TFRA, Louis Kasera, aliwashukuru wadau wote waliochangia na kuwesheza kupatikana tani 78.5 za mbolea. Alisema kiasi hicho kitawasaidia waathirika kuendelea na shughuli zao za kilimo bila shida kwa vile watapokea mbolea za kupandia na kukuzia.

Naye Afisa Kilimo wa Wilaya ya Hanang, Liberatus Msasa, alishukuru kupatikana kwa msaada huo kwa kuwa wilaya yake inategemea kilimo kwa asilimia 80 na kwamba, kwa kiasi kikubwa janga limeathiri sekta hiyo muhimu.

Ameahidi kusimamia ugawaji wa mbolea hizo na kuhakikisha walengwa ndio wanaonfaika na pembejeo hiyo muhimu.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akizungumza na wananchi wa Katesh, Wilayani Hanang (hawapo pichani) alipofanya ziara mjini hapo mnamo tarehe 6 Desemba, 2023 ili kuwapa pole kwa mafuriko ya tope yaliyowakumba na kusababisha vifo na upotevu wa mali mnamo Tarehe 3 Desemba, 2023



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Joel Laurent (wa pili kulia) alikabidhiwa shehena ya mbolea kiasi cha tani 30 na Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni la Mbolea la Taifa (TFC) Samuel Mshoto (Wa pili kushoto) katika kituo cha Kilimo Kilichopo Katesh Wilayani Hanang walipofika ili kutoa msaada ya mbolea kwa wakulima walioathirika na mafuriko ya tope yaliyotokeza tarehe 3 Desemba, 2023 ambapo wadau mbalimbili wa tasnia ya mbolea walijitokeza kuchangia na hivyo kufikisha kiasi cha tani 78.5 za mbolea zilizogawiwa kwa waathirika.



Rais Samia afurahishwa na ongezeko matumzi ya mbolea

Na MWANDISHI WETU

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema ongezeko la matumizi ya mbolea katika klimo ni ishara kubwa kwamba sekta hiyo sasa inaleta tija kwa wakulima.

Amesema kuongezeka kwa uzalishaji kwenye miradi mbalimbali ya kilimo inayosimamia na vijana kupitia mradi wa Kuijenga Kesho iliyo Bora (BBT) chini ya Wizara ya Kilimo ni kipimo cha matumizi mazuri ya mbolea.

Dkt Samia alieleza hayo tarehe Agosti 7, 2023, alipokuwa akizungumza na vijana barani Afrika kuhusu jitihada mbalimbali zin-

azofanywa na serikali mbalimbali katika kuhakikisha vijana wanaingia kwenye shughuli za uzalishaji na kupunguza changamoto inayowakabili ya kukosa ajira.

Alisema ishara nyingine ni kuongezeka kwa mchango utokanao na kilimo kwenye uchumi wa nchi, kiasi cha mazao yanayopele-kwa sokoni pamoja na kushuka kwa gharama za chakula sokoni.

Mjadala huu ni mionganini mwa mijadala mbalimbali iliyo fanyika kuanzia Agosti 5 - 8, 2023, wakati wa mkutano wa Kimataifa wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika ambapo zaidi ya washiriki 4,000 kutoka nchi mbalimbali Afrika walishiriki mkutano huo.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan viongozi wa Serikali na viongozi wa jukwaa la Mifumo ya chakula pamoja na washindi wawili wa Tuzo za Grand Prize, uliowashindanisha Wakulima bora kwa upande wa Vijana wa Bara la Afrika katika Mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika - AGRF 2023, uliofanyika katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere (JNICC), Jijini Dar es salaam tarehe 7 Septemba 2023.

Kwa upande wake, Rais wa Kenya, Dkt. William Ruto, akizungumza katika mkutano huo alisema pamoja na kuwekeza katika teknolojia za kilimo cha kisasa, matumizi sahihi ya mbolea na mbegu husaidia katika kuongenza kipato na kuleta mapinduzi ya kilimo barani Afrika.

Alisema nchi yake inawasaidia wakulima kuongeza uzalishaji wa chakula kwa kuwawezesha kupata mbolea na mbegu kwa bei nafuu.

Kwa mwaka 2023 Kenya ilisajili wakulima 5,000 na kusambaza mbolea kwa kutumia mtandao wa kielektroniki ili kuondoa madalali na matapeli ambao mara zote huwafanya wakulima kupata mbolea kwa gharama kubwa.

Kenya imepunguza gharama ya mbolea kutoka dola 50 hadi dola 20 kwa tani moja. Kupitia kampuni ya mbolea ya YARA Kenya imeongeza kiwango cha utoaji wa mbolea msimu uliopia na hivyo kutegemea kuvuna magunia milioni 44 hadi milioni 61 ya mahindi kutohama na kutumia mbegu bora na kuhakikisha upatikanaji mzuri wa mbolea utakaochochea kupatikana kwa mazao mengi shambani.

Mkutano huo ulihudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwemo Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isidor Mpango na viongozi mbalimbali wa ngazi za juu kitaifa.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa katika mjadala maalum wa vijana uliofanyika katika Ukumbi wa Selous katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere Septemba 7, 2023.

Wakaguzi wa Mbolea watakiwa kuwa waadilifu na weledi



Maafisa kilimo ishirini (zo) kutoka halmashauri mbalimbali nchini, wakifuatilia mada iliyokuwa ikitolewa na Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Udhhibit wa Mbolea Tanzania, Kanda ya Kati, Allan Mariki wakati wa mafunzo ya Utaguzi wa Mbolea yaliyofanyika mkoani Morogoro mwezi Desemba, 2023.



Maafisa kilimo wakipata mafunzo kwa vitendo walipotembelea ghala la mbolea la ETG ili kuwa na uelewa wa namna ya kukagua ubora wa mbolea, mafunzo yaliyotolewa na Afisa Udhhibit Ubora wa Mamlaka, Sostheness Wambura.

Na MWANDISHI WETU

Wakaguzi wa Mbolea nchini wametakiwa kufanya kazi yao kwa uadilifu na weledi mkubwa ili kuhakikisha kuwa mkulima anapata mbolea yenye ubora unaokubalika.

Wito huo umetolewa na Katibu Tawala Msaidizi Uchumi na Uzalishaji wa Mkoa wa Morogoro Dkt. Rozalia Rwegasira leo tarehe 18.12.2023 mkoani Morogoro.

Dkt. Rwegasira amewataka wakaguzi hao, kutenda haki wakati wa utekelezaji wa majukumu yao na kue-puka kabisa vishawishi vyovypote vina-vyoweza kuwaingiza katika rushwa na hivyo kuleta madhara katika Taifa kwa ujumla.

Jumla ya maafisa kilimo zo kutoka halmashauri mbalimbali nchini wanahudhuria mafunzo ya siku tatu kuhusu udhibiti wa mbolea ili kuwajengea uwezo kuwa wakaguzi wa mbolea katika maeneo yao.

Dkt. Rwegasira amesema katika miaka mitano iliyopita Tanzania imekuwa ikitumia tani 300,000 hadi 600,000 za mbolea kwa mwaka ambayo ni sawa na asilimia 30 hadi 60 ya lengo ambalo ni tani millioni moja.

Ameongeza kuwa serikali ya Awamu ya Sita katika msimu wa 2022/2023 na 2023/2024 imeweka mmkakati mahususi wa kuongeza matumizi ya mbolea kwa kutoa ruzuku.

Akizungumza kwa niaba ya Mkrugenzi wa Huduma za Udhhibit, Bwana Allan Mariki amesema Mamlaka imejivekea lengo la kuwa na wakaguzi wawili kwa kila halmashauri ili kuimarisha ufani katika udhibiti wa tasnia ya mbolea nchini.

Mariki amesema mafunzo hayo yanalenga kuwajengea uwezo na kuwapa mbinu sahihi za udhibiti wa ubora wa mbolea kama zilivyoainishwa kwenye Sheria ya Mbolea Na.9 ya mwaka 2009 na kanuni zake.

Aidha, Bwana Mariki amewataka mawakala na wafanyabiashara wa mbolea nchini kutojihusisha na vitemdo vya kuchezza Mfumo wa Mbolea za Ruzuku kwani hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao wote watakao-bainika kufanya hivyo.



Mgeni Rasmi na Naibu Waziri wa Wizara ya Kilimo, David Silinde akiwa katika picha na Wajumbe wa Bodii ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) na watumishi wa Wizara mara baada ya kukabidhiwa tuzo ya mgeni rasmi wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mbolea Duniani yaliyofanyika tarehe 13 Oktoba, 2023 mkoani Tabora

Serikali yataka wakulima kuhakiki taarifa kuhusu mbolea ya ruzuku

Na MWANDISHI WETU

Serikali imewataka wakulima wote nchini waliosajiliwa kwenye mfumo wa ruzuku ya mbolea msimu wa 2022/2023 na kupata namba za kununulia bidhaa hiyo kuhakiki taarifa zao kwenye daftari la mkulima linalopatikana kwenye ofisi za watendaji wa vijiji/mitaa ili kuhaulisha taarifa zao kwa ajili ya kunufaika tena na Mpango wa Ruzuku ya Mbolea kwa msimu 2023/2024.

Wito huo umetolewa na Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde, wakati alipokuwa akiwahutubia maelfu ya wananchi wa Mkoa wa Tabora kwenye kilele cha Siku ya Mbolea Duniani iliyofanyika kwenye Uwanja wa Chipukizi Oktoba 13, 2023 mkoani Tabora.

Aliwataka wakulima ambao hawakusajiliwa kwenye mfumo wa ruzuku ya mbolea msimu wa 2022/2023 wakajisajili kwenye daftari la mkulima ambalo pia linapatikana kwenye ofisi za watendaji wa vijiji/mitaa ili taarifa zao ziingizwe kwenye mfumo na wapate namba itakayowawezesha kununua mbolea za ruzuku kwa msimu wa kilimo 2023/2024.

Silinde aliiagiza Mamlaka ya Mbolea Tanzania (TFRA) kuendelea kusimamia kikamilifu na kuchukua hatua kwa yejote atakayethibitika kufanya kitendo chenye nia ya kuhujumu Mpango wa Utoaji wa Mbolea za Ruzuku kwa wakulima.

"TFRA kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mrajisi wa Vyama vya Ushirika Tanzania na Kampuni za Mbolea haina budi kuhakikisha kwamba vituo vya mauzo ya mbolea vilivyoainishwa vinapangiwa wafanyakishara/vyama vya ushirika vilivyojitekeza kushirikii mpango huu na kuhakikisha kwamba mbolea zinapatikana kwa wakulima katika kipindi chote cha msimu wa kilimo," alisema Silinde.

Pia, waziri huyo alilitaka TFRA kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI kuendelea kutoa elimu ya Mpango wa Ruzuku ya Mbolea, matumizi sahihi ya mbolea na kuhamasisha wakulima kujitokeza katika usajili na uhakiki wa taarifa zao kwenye daftari la mkulima.

Halmashauri za Wilaya pia zilitakiwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kupima afya ya udongo kwenye mashamba ya wakulima kwa ku-

tumia vipima afya ya udongo (soil scanners) vinavyoendelea kusambazwa na Wizara ya Kilimo ili kuwezesha wakulima kutumia mbolea kulingana na mahitaji ya afya ya udongo.

Waziri Silinde alisema kuwa wastani wa matumizi ya mbolea nchini Tanzania unaendelea kuimarika kutokana na kuongezeka kwa uelewa wa wakulima kuhusu umuhimu wa matumizi ya bidhaa hiyo katika uzalishaji wa mazao ya kilimo.

"Hutua hiyo imeendelea kuchangia ongezeko la uzalishaji wa mazao ya kilimo mwaka hadi mwaka. Nitumie fursa hii kuwaponeza wakulima wote nchini kwa kuendelea kuona umuhimu wa sekta ya kilimo kama sehemu ya ajira na kuongeza kipato.

Ninaamini kwamba wakulima wa nchini hii ni wajasiliamali walioamua kujijiri katika kilimo kwa kuwekeza kwenye uzalishaji wa mazao ya kilimo.

Nitoe rai kwa wakulima kuendelea kuzingatia ushauri unaotolewa na maafisa ugani katika kuzingatia kanuni za kilimo bora, ikiwemo matumizi sahihi ya mbolea na mbegu bora," alisema waziri.

Dhamira ya Rais Samia ni kuleta unafuu wa gharama za usambazaji mbolea ya ruzuku



Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan (kulia) akimsikiliza Mwenyekiti wa Bodii ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dk Anthony Diallo, alipotembelea banda la Mamlaka wakati wa kilele cha Maonesho Nanenane yaliyofanyika kitaifa Mbeya. Agosti 8, 2023.

Na MWANDISHI WETU

Katika jitihada za kuhakikisha kwamba wakulima wananaufaika na mpango wa mbolea ya ruzuku, Wizara za Kilimo na Fedha zimepe-wa jukumu la kujadili gharama za usambazaji wa pembejeo hiyo ili kuleta unafuu wa upati-kanaji wake kufikia ngazi ya kata.

Hii ni dhamira ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kama alivypendekeza wakati wa kilele cha Maonyesho ya Wakulima yaliyofanyika mjini Mbeya na kuhitimishwa Agosti 8, 2023.

Gharama ya usambazaji mbolea kufikia ngazi ya kata imekuwa ni changamoto ilijo-tokeza msimu uliopita wa kilimo bei ya mfumo ikiwa ni 70,000/- kwa mfuko lakini ili mbolea imfikie mkulima bei hiyo imekuwa ikipandishwa na baadhi ya mawakala kufikia 85,000/- kwa mfuko.

Hali hii ilimlazimu Rais Dkt Samia kumwanga Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, kuanga-

lia namna ya kupata gharama za usambazaji angalao kwa mawakala wakubwa ili kuleta ahueni kwa wakulima.

Ni agizo la Rais Rais Dkt Samia kwamba Serikali nayo inapaswa ichangie na mkulima mwenyewe naye achangie ili mtu mmoja asi-bebe mzigo peke yake.

Azma ya serikali, kwa mujibu wa Rais, ni kuendelea kutoa ruzuku ya mbolea ili kuongeza uzalishaji wa mazao, huku wakulima wakiendelea kujisajili na kuhakiki taarifa zao za usajili ili kuwezesha kununua mbolea hiyo.

Rais Samia amekuwa kisisitiza kuywa ajenda ya Serikali ni kuongeza mchango wa sekta ya kilimo hadi asilimia 10 ifikapo mwaka 2030 na kwamba uwerekano huo upo.

Mkazo wa serikali pia ni kuelekeza ngu-vu zake katika sekta za uvuvi na ufugaji kwa kuongeza bajeti ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

"Lengo la Serikali ni kutumia hekta mili-ioni 29.4 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliani

ambapo kwa sasa zaidi ya hekta 700,000 ndizo zinazotumika katika umwagiliani na milioni 28 zimebaki," anasema Rais.

Ili kufanikisha uzalishaji katika kilimo, uvuvi na ufugaji, Rais amekuwa akiwataka maofisa ugani kukaa katika maeneo waliyopangiwa ili kuwasaidia wakulima na wafugaji kwa ku-wapatia utalaamu na mbinu za kisasa za uzalishaji.

Katika Maonyesho ya Wakulima Mbeya, Mbunge wa Mbeya Mjini Dk Tulia Ackson naye alipendekeza Maonyesho Nanenae yawe yaki-fanyika kwa wiki mbili ili kutoa fursa kwa wananchi kufanya biashara zao hadi pale mamlaka zitakapoanza mchakato wa kuboresha viwanja vya maonyesho.

Ni pendekoz ambalo Rais aliliridhia. "Naungana na Spika (Dk Tulia) kutoa wiki moja zaidi kwa wawezesaji hasa wale waliotoka Nyanda za Juu Kusini ili kuendelea kuonyesha na kuchukua vifaa. Nimwagize Bashe aongeze siku nyininge saba," alisema.

Wanamichezo TFRA wakabidhi vikombe kwa menejimenti



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania, Joel Laurent (mwenye koti la kaki) akiwa amenyanya ukiKombe la ushindi wa kwanza kwa mchezo wa pool table alipokabidhiwa na Mkurugenzi wa Huduma za Mamlaka, Victoria Elangwa (kushoto kwake).



Wafanyakazi wa TFRA walioiwakilisha Mamlaka kwenye michezo ilioandalika na Shirikisho la Michezo ya Mashirika, Taasisi za Umma na Sekta Binafsi (SHIMMUTA) iliufanyika kuanzia Dodoma Novemba 2023.

Na MWANDISHI WETU

Washiriki wa michezo ilioandalika na Shirikisho la Michezo ya Mashirika, Taasisi za Umma na Binafsi (SHIMMUTA) wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) walikabidhi vikombe viwili nya ushindi wa kwanza walivyovitwa katika michezo ya pool table na kukimbia ndani ya gunia.

Mkurugenzi wa TFRA Joel Laurent aliwapongeza washindi hao kwa kuitetea taasisi na kuipa heshma katika michezo hiyo.

Alifurahiswa na uamuzi wa Mamlaka na watumishi kujipanga kushiriki michezo hiyo ya SHIMMUTA iliufanyika jijini Dodoma, ambapo TFRA ilikuwa mionganoni mwa taasisi 53 zilizoheshimu uamuzi ya Serikali ya kuruhusu watumishi kushiriki michezo ya SHIMMUTA yenye lengo la kuboresha afya.

Laurent alisema Mamlaka itajipanga kuhakikisha inaonegeza ushiriki wa watumishi katika michezo hiyo kwa kuboresha eneo la watumishi kufanya mazoezi na kutenga babeti ya michezo.

Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi wa TFRA, Victoria Elangwa, aliwapongeza washindi kwa uamuzi wa kukaa sehemu moja na kufanya mazoezi wakati wote wa mashindano hayo.

"Kitu kizuri walikaa pamoja na ikawa rahihi kujuliana hali na kufanya mazoezi kwa pamoja. Ni jambo zuri sana," alisema Elangwa.

TFRA ilishiriki michezo ya ndani ijuikanayo kama michezo ya jadi ikiwa ni pamoja na pool table, kukimbia ndani ya gunia, karata, bao, draft na kurusha vishale.

Katika michezo yote Mamlaka ilifanikiwa kufika robo fainali na kuwa mshindi wa kwanza katika michezo ya pool table na kukimbia ndani ya gunia.

"Mwaka jana TFRA ilishiriki kwa mara ya kwanza na kufanikiwa kurudi na ubingwa kwenye michezo wa pool table.

Akifunga michezo hapo Novemba 25, 2023, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Rosemary Senyamule alizipongeza taasisi zote zilizoshiriki katika michezo hiyo ambayo ilikuwa ni fursa nzuri kwa wakazi wa jiji hilo.

Aliahidi kuwapa eneo wana-SHIMMUTA la kujenga uwanja wa michezo kufuatia maombi yaliyotolewa na Mwenyekiti wa shirikisho hilo, Roselyne Massama.

Alisema michezo ya SHIMMUTA iliufanya Dodoma kuchangamka na kuwa fahari ya Watanzania na kuwataka wadau wengine kufanya shughuli zao katika mkoa huo ikiwemo michezo.

Aliyataka mashirika na taasisi nyingine za serikali na binafsi zisiwanyime nafasi wafanyakazi wao kushiriki katika michezo mbalimbali kwa ajili ya kutunza afya zao.

Namna matumizi ya mbolea yanavyostawisha vitunguu maji



Na AZIZ MTAMBO

UWEKAJI MBOLEA katika mmea wa kitunguu ni muhimu kwa kwa sababu vitunguu vinahitaji hewa ya nitrojeni zaidi. Vitunguu vinahitaji matumizi ya virutubishi kwa wakati kwa ajili ukuaji na tija ya mmea wenywewe.

Vitunguu hunufaika kutokana na urutubishaji unaofaa (ikitegemea matokeo ya majoribio ya udongo), ingawa mbolea za nitrojeni nyingi zinapaswa kutumiwa kwa tahadhari. Nitrojeni kupita kiasi inaweza kuchelewesha uundaji wa balbu, kukomaa na kuhifadhi vitunguu.

Zaidi ya hayo, mizizi ya vitunguu huzuiliwa kwenye udongo wa juu wa inchi 18, na hivyo kufanya iwe vigumu kusambaza virutubisho vya mazao. Upimaji wa udongo katika kilimo cha vitunguu ni muhimu, pamoja na kuchagua mbegu bora.

Matokeo ya majoribio ya udongo, uzoefu wa shambani na mahitaji mahsusii ya mazao yanaweza kusaidia kubainisha virutubisho muhimu na viwango vya matumizi ya mbolea yanayohitajika.

Mpango wa lishe bora wa mazao unaweza kusaidia kuboresha mavuno kwa ujumla kwa kuongeza uzito wa balbu za kitunguu.

Naitrojeni huongeza mavuno ya vitunguu - Kiwango cha juu cha nitrojeni ni muhimu kwa uzito wa kitunguu. Aidha, nitrojeni husaidia

kuzalisha majani hivyo idadi ya majani huongeza ukubwa wa balbu.

Boroni huathiri uzito wa balbu - Majoribio yanathibitisha kwamba boroni ina athari chanya kwenye uzalishaji wa Kitunguu kwa kuongeza uzito wa balbu. Ni muhimu kudumisha uwiano sahihi wa nitrojeni, kalsiamu na boroni kwenye udongo, kwani kalsiamu nyiningi na viwango vya juu vya nitrojeni vinaweza kupunguza kiwango cha boroni.



Mbolea za NPK (Naitrojeni, fosiforasi na Potashi)

Naitrojeni ni kirutubisho muhimu kwa ukuaji wa vitunguu. Zao la kawaida la Kitunguu hutumia takriban kilo 100 za nitrojeni halisi kwa hekti wakati wa msimu wa kupanda, na nitrojeni nyingi hu-chukuliwa baada ya balbu za mimea kupandwa. Mbolea ya nitrojeni huwekwa pemberi ya mmea/shina kwa kutumia kiasi kidogo ili kue-puka kuchoma mimea.

Kwa nini vitunguu vinahitaji nitrojeni?

Mbolea za Naitrojeni zitaongeza ukubwa wa majani ya kitunguu na, kwa sababu hiyo, kuongeza majani (scales) ya balbu, na kuifanya kuwa kubwa zaidi. Kwa lengo la soko, Vitunguu vikubwa vinaweza kuongeza mapato ya biashara. Ingawa, mbolea ya nitrojeni pekee haiwezi kutoa mavuno mengi, Unahitaji kununua mbolea ambayo kemikali yake ni pamoja fosforasi. Kabla ya kupanda, kwanza unahitaji kupima udongo. Ikiwa udongo una viwango vya chini vya fosforasi ya asili, utahitaji kuongeza fosforasi ili kusaidia kuongeza mavuno.

Ni muhimu kuzuia utumiaji mwingu wa naitrojeni kucheleta (katikati ya msimu) na baada ya balbu kuanza, kwani itahimiza kumoa kwa kucheleta na kuweka shingo kubwa, ambazo ni ngumu kutibu. Zaidi ya hayo, Naitrojeni iliyozidi kwenye balbu italainisha balbu za Vitunguu na uhifadhi duni wakati wa kuvuna. Vitunguu vinahitaji nitrojeni ya wastani, lakini urutubishaji wa Naitrojeni bado ni muhimu kwa sababu Vitunguu vina mfumo dhaifu wa mizizi.

Fosforasi na potasiamu

Vitunguu vinahitaji viwango vya juu vya potasiamu na fosforasi. Mbolea hutoa virutubisho hivi kwa namna ya potashi na Fosfati. Fosforasi ni muhimu kwa ukuaji wa mapema wa mmea. Kwa hiyo, ikiwa kiasi cha fosforasi kitatumwa wakati wa kupanda, unapaswa kuweka inchi mbili chini ya mbegu. Vitunguu vinahitaji potasiamu ya wastani.



Fosforasi ni muhimu kwa ubadilishaji wa wanga (Carbohydrate), kimetaboliki ya protini, (protein metabolism) na fosforasi (phosphorylation). Upungufu wake husababisha ukuaji usiofaa na ukuaji duni wa balbu za Kitunguu. Potasiamu ni muhimu kwa shughuli nzuri ya usanisinuru (photosynthetic activity), uhamaji, na utumiaji wa wanga wa sintetiki (synthetic carbohydrates). Upungufu wake husababisha majani ya manjano - kijani, sehemu za juu, na balbu ndogo kukauka.

Kilimo cha vitunguu kinahitaji kilo 100 za nitrojeni, kilo 50 za fosforasi, na potashi kilo 50 kwa hekti. Aidha, salfa pia ni kirutubisho muhimu kwa mavuno bora.

Virutubisho vidogo katika Vitunguu (Micronutrients)

Ingawa virutubishi vidogo sana vinahitajika ili kukidhi uzalishaji wa Vitunguu, uwiano sahihi wa vipengele hivi vya ufuatiliaji ni muhimu. Virutubisho muhimu zaidi ni boroni na chuma (Iron). huongeza tija na ubora. Zinki pia ina jukumu katika kuota kwa mbegu.

Matumizi bora ya mbolea kupata Vitunguu vikubwa

Mbali na mbinu sahihi za urutubishaji na umwagiliaji, uchaguzi wa aina za Vitunguu ni jambo muhimu katika kukuza Vitunguu vikubwa. Superphosphate hufanya kama mbolea ya kuanza, kuhimiza mizizi imara na mapema. Usitumie mbolea baada ya katikati ya majira ya joto (after mid-summer). Utumiaji wa mbolea uliochelewa huhimiza ukuaji mpya, laini, na Vitunguu havitaishi. Mbali na mbolea sahihi, Vitunguu vinahitaji udongo wenye unyevu sawa ili kukua.



Funika udongo kwa vipande vya nyasi ambavyo havijatibwa ili kuhifadhi unyevu. Sambaza vipande vya nyasi vya inchi 1/4 kwenye udongo kila wiki, na acha vipande vikauke kabla ya kuongeza vingine.

Njia rahisi zaidi ya mbolea ya vitunguu.

Vitunguu ni zao ambalo hutumia virutubisho kwa wingi (heavy feeder) na ina mizizi midogomidogo (sharrows roots), hivyo mbolea sahihi ni muhimu kwa mazao ya Vitunguu. Rutuba ya kutosha ya udongo ni muhimu katika maeneo ambayo Vitunguu hukua haraka kabla ya balbu kuunda kutokana na kupungua kwa urefu wa siku.

Mbolea ya kupandia

Mbolea hizi huwekwa kabla au mara ya tu baaada ya kuhamishia miche shambani. Mbolea hizi zina lengo la kusaidia ukuaji mzuri wa mifumo ya mizizi (root system) itakoyosaidia mmea kufonza virutubisho na maji kutoka ardhini.

Mbolea hizi zina kirutubisho kikuu cha fosforasi na huitwa mbolea za fosfati (phosphate Fertilizer), kundi hili lina mbolea kama MAP, TSP, DAP, Minjingu nk.

Mbolea za kukuzia



Mbolea hizi huwekwa kipindi cha ukuaji wa mmea (vegetative growth) na hua na lengo la kuupa mmea ukuaji mzuri utakaopelekea kua na majani mazuri yatakayotegemea chakula cha kutosha kwenye mmea.

Mbolea hizi huwekwa wiki tatu mpaka sita baada ya kupanda miche ya vitunguu shambani.

Weka mifuko mitatu wiki ya tatu au mifuko mine wiki ya sita (kwa kila hektaa moja), kumbuka kwamba kila shina moja linahitaji kijiko kimoja cha chai/kisoda kilichojaa mbolea ya kukuzia, hakikisha pia mbolea haigusi shina la mmea hivyo weka pembeni karibu na mmea kuepusha kuunguza shina la mmea huo.

Kitendo hiki mmea kutengeneza chakula chake huitwa Usanis-inuru (Photosynthesis) na hufanyika kwenye majani. Kirtubisho kikuu katika hili la mbolea ni Naitrojeni (N). Baadhi ya mbolea zilizopo kwenye kundi hili ni pamoa na UREA, SA, CAN nk.

Pia kwenye kundi hili zipo mbolea za maji zinazopiga kwenye majani (Foliar fertilizers) hujulikana pia kama booster.

Mbolea za kuzalisha/kukomazia kitunguu



Uwekaji wa mbolea za maji

Hizi ni zile zinazowekwa kuusaidia mmea kutengeneza kitunguu (bulb formation). Kirutubisho kikuu hapa ni Potasiamu (Potassium). Ili kitunguu kiweze kujijenga vizuri na kua na ubora mzuri kinahitaji mbolea zenye kirutubisho cha Potasiamu (Potassium). Mfano wa mbolea zenye virutubisho hichi ni Multi K, MOP (Muriate of Potash) nk.

Hayo ndio makundi makuu ya mbolea, japokuwa mbolea hizo hujumuisha pia virutubisho vidogo (micronutrients) ambavyo vinahitajika kwa udongo kwenye mimea, japokuwa zina kazi muhimu kwenye mmea.

Vitunguu haviwezi kufikia ubora wake bila kuweka virutubisho vidogo kama vile shaba(coper), manganisi na zinki. Njia rahisi zaidi ya kuhakikisha kuwa udongo wako una madini haya ni kutumia urekebishiwa wa virutubisho vidogo (micronutrient modification) kama vile azomite au unga wa kelp kwa 0.453592 Kg hadi 0.907184 Kg kwa futi 100 za mraba.

Vidokezo vya kuchagua mbolea nzuri kwa vitunguu

Vitunguu vinahitaji udongo wenye lishe ili kustawi. Kutumia mbolea sahihi kutakuza ukuaji wao na kusaidia mmea kukua balbu kubwa na zenye afya. Ili kuchagua mbolea inayofaa kwa zao la Kitunguu, unapaswa kuzingatia asilimia ya Naitrojeni, fosforasi (fosforasi), na potasiamu (potashi) katika bidhaa, ambayo kwa kawaida huitwa NPK.

Unapaswa kuchagua mbolea iliyochanganywa na kiwango kikubwa cha Naitrojeni kwa zao la Kitunguu. Huongeza mavuno na kuboresha ubora, uhifadhi, na ukinzani wa magonjwa.

Tambua na uchunguze ikiwa Vitunguu vyako vina upungufu wa virutubishi, na unapaswa kujua kuhusu dalili na sababu na jinsi ya kudhibiti au kurekebisha upungufu huu.

Upungufu wa nitrojeni



- Dalili – Majani yaliyozeeka kuwa ya manjano. Kudumaa kwa ukuaji.
- Utatuza – weka mbolea ya maji ya urea 1% au DAP 2% mara mbili kwa wiki.

Upungufu wa fosforasi



- Dalili: Ukuaji wa polepole. Majani yanageuka kijani kibichi, na balbu zina maganda makavu ya nje, pia shingo nene.
- Utatuza – Kiwango kinachopendekezwa cha fosforasi kwenye udongo kinapaswa kutumika wakati wa kupanda. Nyunyizia DAP 2% kwenye majani mara mbili kwa muda wa siku 15.

Upungufu wa potasiamu

Dalili: Kwa sababu potasiamu ina nguvu nyingi katika mimea, dalili za upungufu mkubwa huonekana kwenye majani machanga pekee. Dalili za kuungua kwa ncha (Kuungua kwa pembe za majani) Majani huwa kijani kibichi. Majani ya zamani yanageuka manjano, na shingo kuwa na michubuko (bruised)

- **Utatuizi:** Utumiaji wa mbolea za maji (foliar) wa $K_2SO_4 @ 1\%$ mara mbili kwa wiki.

Vitunguu haviwezi kufikia ubora wake bila kuweka virutubisho vidogo kama vile shaba(coper), manganese na zinki. Njia rahisi zaidi ya kuhakikisha kuwa udongo wako una madini haya ni kutumia urekebishaji wa virutubishi vidogo (micronutrient modification) kama vile azomite au unga wa kelp kwa 0.453592 Kg hadi 0.907184 Kg kwa futi 100 za mraba.

Maswali yanayoulimiza mara kwa mara (FAQ) kuhusu mbolea ya vitunguu

**Ni mbolea gani bora ya vitunguu?**

Vitunguu vinahitaji vyanzo vingi vya nitrojeni ambayo huwekwa wakati wa kupanda na kuota na badaye katika hatua ya ukuaji.

Je, mbolea ya urea inafaa kwa vitunguu?

Urea huchochea kwa kiasi kikubwa ukuaji wa Kitunguu, uzalishaji na vitaminini C.

Je, urea inafaa kwa vitunguu?

Kwa hiyo, urea foliar inaweza kupendekezwa ili kuimarisha ukuaji wa Vitunguu

Je, vitunguu vinahitaji fosforasi?

Vitunguu vinahitaji viwango

vya juu vya potasiamu na fosforasi. Mbolea hutoa virutubisho hivi kwa namna ya potashi na phosphate. Ombo takriban gramu 63 za fosfeti na 137gramu potashi kwa kila futi 100 za mraba.

Kwa nini vitunguu vyangu ni vidogo sana?

Kupanda aina tofauti za Vitunguu visivyoofaa kwa hali ya hewa yako kutasababisha vitunguu vidogo. Aidha, kutokana na mabadiliko ya joto, Kitunguu huwa kidogo kutokana na kutoa maua mapema. Ukosefu wa virutubisho kutokana na ushindani au udongo duni husababisha Vitunguu vidogo.

Kona ya Sheria



Mwenyekiti wa Bodii ya wakurugenzi wa Mamlaka ya Udhiliti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dkt. Anthony Diallo akiwa na baadhi ya wajumbe wa bodi hiyo akizungumza wakati wa kikao kifupi na uongozi wa mpaka wa Tunduma na Malawi kilicholenga kujadili namna nzuri ya kuongeza udhibiti wa utoroshwaji wa mbolea unaofanyika mipakani. Pamoja na kusikiliza za changamoto wanazokutana nazo wakati wa kukagua bidhaa za mbolea zinazopitia katika bandari hiyo Kwenda nchi Jirani tarehe 17 Oktoba, 2023.

Ijue sheria ya Mamlaka ya Udhiliti wa Mbolea Tanzania

Na MWANDISHI WETU

Utangulizi

Mamlaka ya Udhiliti wa Mbolea Tanzania (TFRA) ni taasisi ilio chini ya Wizara ya Kilimo ilioanzishwa kwa Sheria Na. 9 ya Mwaka, 2009. Mamlaka ilianza kutekeleza majukumu yake Agosti, 2012. Jukumu kuu la Mamlaka ni kudhibiti ubora wa mbolea kwa kusimamia biashara ya mbolea katika mnyororo wa thamani ikiwemo utengenezaji, uingizaji nchini, usafirishaji nje ya nchi, uuzaaji na matumizi ya mbolea kwa ajili ya kilimo kwa lengo la kuhakikisha mbolea inayomfikia mkulima ina ubora unaokidhi viwango.

Majukumu

Mamlaka katika kutekeleza majukumu yake inaongozwa na Sheria ya mbolea. Sheria ya mbolea ambayo inaweka masharti ya utengenezaji, uingizaji nchini, usafirishaji nje ya nchi, uuzaaji na matumizi ya mbolea kwa ajili ya kilimo. Aidha, kifungu cha 4(1) cha Sheria kimeainisha majukumu mahususi ambayo kwa ujumla wake yanafanikisha utekelezaji wa jukumu kuu ambaloni udhibiti ubora wa mbolea.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 4(1) Mamlaka itakuwa chombo cha udhibiti katika tasnia ya mbolea na kipekee-

(a) itadhibiti masuala yote yanayohusi-

Mamlaka katika kutekeleza majukumu yake

inaongozwa na Sheria ya mbolea. Sheria ya mbolea ambayo inaweka masharti ya utengenezaji, uingizaji nchini, usafirishaji nje ya nchi, uuzaaji na matumizi ya mbolea kwa ajili ya kilimo.

ana na ubora wa mbolea, visaidizi vya mbolea na mitambo ya utakasaji;

(b) itasajili wafanyabiashara wote wa mbolea na visaidizi vya mbolea na maeneo yao;

(c) itatoa leseni kwa wafanyabiashara wa mbolea;

(d) itatoa vibali kwa ajili ya mbolea na visaidizi vya mbolea kuingizwa nchini na kusafirishwa nje ya nchi;

(e) itatunza rejestra ya mbolea na visaidizi vya mbolea, mitambo ya utakasaji na viwanda vya kutengeza mbolea;

(f) itatunza na kutangaza mara kwa mara rejestra ya wafanyabiashara wa mbolea;

(g) itakeleza mikataba ya kimataifa ili-yordihwa kuhusiana na mbolea;

(h) itadhibiti na kusimamia uingizaji nchini, uzalishaji, usafirishaji nje ya nchi, ushughulikiaji, uhifadhi, na uteketezaji wa mbolea au visaidizi vya mbolea;

(i) itakusanya, kutunza na kuchapisha taarifa zinazohusiana na mbolea na kisaidizi cha mbolea;

(j) itaandaa miongozo juu ya usimamizi sahihi na udhibiti wenye ufanisi wa mbolea na visaidizi vya mbolea;

(k) kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa, itafanya makongamano ya kutoa elimu kwa umma juu ya matumizi sahihi na usimamizi wa mbolea na visaidizi vya mbolea;

(l) itatoa mafunzo ya mara kwa mara kwa wadau kuhusu masuala ya mbolea;

(m) itasajili wakaguzi na wachambuzi;

(n) itakagua au kuwezesha ukaguzi wa mbolea au visaidizi vya mbolea kwa ajili ya kujihakikisha ubora;

(o) itakeleza sera, mikakati na mipango inayohusiana na maendeleo ya tasnia ya mbolea;

(p) itatoa ushauri wa kitaalamu kwa Serikali na taasisi zingine katika masuala yote yanayohusiana na usimamizi na udhibiti wa mbolea na visaidizi vya mbolea;

(q) itafanya au kuwezesha kufanyika utafiti kuhusiana na mbolea na visaidizi vya mbolea;

(r) itakuza ushirikiano kati ya taasisi na taasisi nyingine au mashirika na wadau;

(s) itashirikiana na mashirika ya kitaifa na kimataifa kwenye masuala yote yanayohusiana na mbolea na kisaidizi cha mbolea;

(t) itatekeleza maelekezo maalum na ya ujumla ya Mamlaka;

(u) itadhibiti bei ya mbolea kwa kuzingatia njia sahihi kama zitakavyoinishwa katika kanuni;

(v) itaainisha njia au mfumo sahihi wa uingizaji nchini na usafirishaji nje ya nchi wa mbolea au visaidizi vya mbolea;

(w) itatekeleza majukumu mengine yoyote kama inavyowenza kupewa katika utekelezaji wa majukumu chini ya Sheria hii; na

(x) itahakikisha kwamba inazingatia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

Wadau wataka yafanyike maboresho Siku ya Mbolea Duniani 2024

Na MWANDISHI WETU

WASHIRIKI wa Maonesho ya Siku ya Mbolea Duniani wamependekeza kuwa Mamlaka ya Udhibiti Mbolea Tanzania ifanye jitihada za makusudi kuyatangaza maonesho ya Siku ya Mbolea 2024 ili kuvutia ushiriki wa wakulima wengi nchini.

Hilo ni moja ya mapendekezo kadhaa yaliyotolewa na washiriki wa maonesho ya Siku ya Mbolea Duniani 2023 yaliyofanyika kitaifa mkoani Tabora Oktoba mwaka huu.

Wakitoa maoni yao kuhusu namna ya kuboresha maonesho hayo yanayofanyika kila mwaka ili kuhamasisha wakulima kutumia mbolea kuongeza tija katika kilimo, washiriki hao kutoka makundi mbalimbali ya wadau kilimo, pia walitaka muda wa maonesho hayo uongezwe kuwa wiki moja badala ya siku mbili tu.

Walisema kuongeza kwa muda kutawapa fursa wananchi wengi kushiriki kikamilifu katika maonesho, hasa suala la kupata elimu kuhusu matumizi ya mbolea.

Walipendekeza hamasa ya maandalizi ya maonesho hayo ianze mapema ili kuvuta idadi kubwa ya washiriki kutoka maeneo mbalimbali vijiji.

"Nguvu kubwa itumike katika uhamasishaji juu ya umuhimu wa maonesho kwa wakulima ili kupata idadi kubwa ya wahudhuriaji," washiriki walipendekeza.

Hali kadhalka, washiriki hao walipendekeza maonesho yafanyike kwenye wilaya na jitihada zifanyike kuwasaidia wakulima wapate nafasi ya kuhudhuria.

Siku ya Mbolea Duniani ni jukwaa muhimu la kuwaunganisha wadau wa tasnia ya mbolea na kilimo kwa ujumla wake.

Juhudi za serikali za kuadhimishwa siku ya

Mbolea Duniani zina lengo la kuimarisha tasnia ya Mbolea ili iweze kutoa mchango wake katika kuongeza kipato cha mkulima na kuchocha upatikanaji wa bidhaa za viwanda zitokanazo na sekta ya kilimo.

Kamati ya Mamlaka ya Udhibiti Mbolea Tanzania iliyoratibu mapendekezo hayo ya wadau ilipendekeza, pamoja na mambo mengine, kutafutwa kwa wadau wa mbolea kitaifa na kimataifa ili waweze kuchangia baadhi ya gharama za maadhimisho ya Siku ya Mbolea Duniani, na kwamba maadhimisho hayo yaambatane na ufunguzi wa msimu wa kilimo Tanzania.

"Kamati ihakikishe inatenga bajeti kwa ajili ya uhamasishaji na kualika wasanii wenye mvuto kwenye jamii ili kuongeza hamasa kwa wananchi kufika kwenye viwanja yanapofanyika maadhimisho ya Siku ya Mbolea Duniani," Kamati ilipendekeza.



Naibu Waziri wa Kilimo, Mhe. David Silinde akitoa maelekezo ya Serikali kwa Mkuu wa Kitengo cha Masoko wa kampuni la uchimbaji madini Minjingu, Dkt. Msolla Mshinda, alipotembelea banda la kampuni hiyo wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mbolea Duniani yaliyofanyika Mkoani Tabora tarehe 13 Oktoba, 2023.

TFRA yasajili wakulima wapya 382,252

Na MWANDISHI WETU

Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2023 imefanikiwa kusajili wakulima wapya 382,252 ambao watanufaika na mpango wa ruzuku ya mbolea kwa msimu wa kilimo 2023/2024.

Hayo yameelezwa na Kaimu Mkurugenzi Uzalishaji wa Ndani na Ununuzi wa Mbolea Kwa Pamoja wa TFRA, Louis Kasera alipokuwa akiwasilisha taarifa ya kipindi cha Julai hadi Disemba 2023.

Kasera amesema azma ya serikali ya kukuza na kuimarisha sekta ya kilimo kupitia utekelezaji wa Mpango wa Mbolea ya Ruzuku sasa imezaa matunda kwani kuna ongezeko la usajili wa wakulima, wafanyabiashara wa mbolea, waingizaji na wazalishaji.

Kasera amesema katika nusu ya kwanza ya msimu wa 2023/2024 wakulima 889,707 walinafaika na mbolea ya ruzuku, ambapo wakulima 161,708 walikuwa ni wapya ambao hawakunufaika na mbolea ya ruzuku katika msimu wa

2022/2023.

